**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**

*(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)*

**Kumb. Na. UA/F.20 VOL.II/64** **06/01/2026**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea anawatangazia watanzania wenye sifa za kuomba nafasi za kazi tatu (03) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

### 1.0 DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 3

### 1.1.1 MAJUKUMU NA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
vi. kufanya usafi wa gari, na
vii. kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

### 1.1.2 SIFA ZA WAOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika. Vilevile, awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA

**TGS B**

**MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka 45,

ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha Kuzaliwa,

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye Anwani, Namba za Simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika,

iv. Waombaji wote waweke nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya Kidato cha Nne na Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika kwenye ***Ajira Portal,***

v. ***Testimonials “Provision Results”, “Statement of Results” Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita HAVIKUBALIKI,***

vi. Waombaji wa kazi ya Kada ya Dereva II wenye Leseni Daraja E au C wanapaswa **KUAMBATISHA** vyeti vya mafunzo ya Udereva vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika.

vii. Waombaji wote waweke picha mbili *“Passport Size*” ya hivi karibuni katika ukurasa wa *Ajira Portal*,

viii. Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuthibitishwa na mamlaka husika yaani TCU, NECTA na NACTE,

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi,

x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka wenye Kumb. Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010,

xi Uwasilishwaji taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria,

xii. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 19 **Januari, 2026.**

xiii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, Anwani ya barua hiyo ielekeze kwa:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa ya Songea,
4Brabara ya Sokoine,
S.L.P 14,

**57101 SONGEA- RUVUMA**

Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira **(Recruitment Portal)** kupitia anuani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal').

xv. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA**.

Limetolewa na:

**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**